**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

# 03 MAARIFA YA JAMII

**Muda: Saa 1:30** **Mwaka: 2020**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **manne (4).**
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.

## SEHEMU A (Alama 28)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Jibu kipengele cha (i) – (viii) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuaiandika katika kisanduku.

(i) Kwanini kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania?
A. Kinapendwa na watu wengi
B. Kinavutia watalii wengi
C. Kinaajiri watu wengi
D. Kinavutia uchimbaji wa madini [ ]

(ii) Nchi ya Tanzania inafaidika vipi na uchimbaji wa madini?
A. Kupata fedha za kigeni C. Kuongezeka kwa mifugo
B. Kuongezeka kwa mazao D. Kuongezeka kwa misitu [ ]

(iii) Ni athari ipi ya uharibifu wa mazingira haisababishwi na uchimbaji wa madini?
A. Ukataji wa miti hovyo C. Uchafuzi wa maji
B. Ongezeko la mvua D. Kuwepo mashimo makubwa [ ]

(iv) Ipi ni faida ya mbuga za wanyama nchini Tanzania?
A. Kuongeza pato la Taifa C. Kuongezeka kwa uwindaji haramu
B. Kupata samadi ya kilimo D. Kupata ardhi nzuri ya kilimo [ ]

(v) Ni kwa nini matumizi ya baruti na sumu hayakubaliki katika shughuli za uvuvi?
A. Huua samaki wengi kwa wakati mmoja
B. Huwapa wavuvi hasara kubwa
C. Hunasa samaki wakubwa tu
D. Husababisha wavuvi kukosa ajira [ ]

(vi) Ni madini yapi yanapatikana nchini Tanzania tu?
A. Tanzanaiti B. Dhahabu C. Almasi D. Chokaa [ ]

(vii) Nini kifanyike ili



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

kurekebisha eneo lililoathiriwa na shughuli za uchimbaji wa madini?

A. Kufuga mifugo wengi
B. Kusafisha ardhi
C. Kumwagilia maji
D. Kupanda miti [ ]

(iv) Ni fursa ipi ya uchumi inayotokana na misitu?

A. Uzalishaji wa nafaka
B. Shughuliza uvuvi
C. Shughuli za urinaji asali
D. Uchimbaji wa amdaini [ ]

2. Jibu kipengele cha (i) – kwa kuoanisha maelezo ya vifaa vinavyotumika kupima hali ya hewa katika **Fungu A** na majina ya vifaa husika katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| Fungu A | Herufi | Fungu B |
|---|---|---|
| (i) Kifaa kinachotumika kupima uelekeo wa upepo. | | A. Haigromita |
| (ii) Kifaa kinachotumika kupima Unyevuanga. | | B. Kampbeli stok |
| (iii) Kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa. | | C. Kipimajoto |
| (iv) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi. | | D. Kipima upepo |
| (v) Kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo. | | E. Kipima mvua |
| (vi) Kifaa kinachotumika kupima mwanga wa jua. | | F. Anemomita |
| | | G. Baromita |
| | | H. Stevenson screen |

## SEHEMU B (Alama 22)

3. Soma majadiliano yafuatayo kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

**Dihenga:** Hujambo?
**Masatu:** Sijambo.
**Dihenga:** Hivi wewe ni kabila gani? **Masatu:** Mimi ni Msukuma, wewe je? **Dihenga:** Mimi ni Mzaramo.
**Masatu:** Nimesikia jana ulikuwa unacheza ngoma katika sherehe
**Dihenga**: Ndiyo tulikuwa tunacheza ngoma iitwayo mdundiko. Wewe hupendelea ngoma gani?
**Masatu:** Na mimi pia napenda mdundiko kwa



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

sababu mwili unakuwa imara

**Dihenga:** Je unapendelea kusalimia watu katika jamii yako?

**Masatu:** Ndiyo mara nyingi ninasalimia watu mbalimbali katika jamii yangu.

**Dihenga:** Mnasalimianaje katika jamii yako?

**Masatu:** Tunasalimiana kwa kushikana mikono, wewe je?

**Dihenga:** Mimi napenda kusalimiana kwa kukumbatiana.

**Masatu:** Ooh! Hongera.

**Dihenga:** Ahsante.

**Maswali:**

(i) Masatu ni kabila gani? ______________

(ii) Dihenga hupendelea kusalimianaje? _________________

(iii) Taja aina ya ngoma wanayocheza Wazaramo _________

(iv) Kwa mujibu wa majadiliano hayo, ni kabila gani husalimiana kwa kushikana mikono? ___

(v) Taja faida ya kucheza ngoma ya 'mdundiko'


(vi) Mazungumzo kati ya Masatu na Dihenga yalianzaje? _______

(vii) Umejifunza nini kutokana na majadiliano hayo? _________

4. Je, alama zifuatazo zinawakilisha nini katika ramani?

(i)  ____________________

(ii)  ____________________

(iii)  ____________________

(iv)  ____________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org